

Changanya mbegu mkono moja na fatalaiza aina ya superphosphate mikono miwili.



Ikiwa huwezi kununua fatalaiza basi changanya mbegu na udongo nyororo. Panda ndani ya mitaro na ufunike kwa udongo.



Palilia baada ya wiki sita. Endelea kupunguza matawi ili isimée kati ya mimea ya mahindi.



Desmodium ya kijani kibichi inaweza pia kudhibiti kwekwe ya striga katika mtama

### **Wakati gani na jinsi gani tunavuna mbegu za desmodium?**

Vuna mbegu kila wiki pindi maganda yakiwa rangi ya kahawia (Brown). Chuma maganda kwa mkono na uweke mbegu ndani ya mkebe.



Kausha mbegu kwa juu kisha twanga kwa jiwe.




Pepeta mbegu ili uondoe uchafu wote.



Hifadhi mbegu zako ndani ya debe au ndani ya chombo kisicho ruhusu hewa kuingia katika mahali pakavu.

### **Mbegu ya desmodium ina bei nzuri kwa hivyo, uza mbegu zako sokoni**

Imetayarishwa na Mediae  
mediae@africaonline.co.ke. Tel 4442660



# **Kuza Desmodium na Uzuie Kwekwe ya Striga**



**Panda desmodium pamoja na mahindi ili izuie kwekwe ya striga kukuwa ndani ya shamba lako la mahindi**

International Centre of Insect Physiology na Ecology (ICIPE), na Rothamsted - Research KARI na Wizara ya Kilimo, Kenya  
Wadhamini: Gatsby Charitable Foundation UK

**Je, umewahi kuona kwekwe hii ndani ya shamba lako la mahindi?**

Kwekwe iitwayo striga.



### **Striga inaweza kuadhiri mazao yako namna gani?**

Striga inaweza kusababisha upotetu wa nusu ya mazao yako. Ikiwa hapo awali ulikuwa unavuna magunia kumi ya mahindi utavuna magunia tano tu, shamba lako likivamiwa na striga.

### **Kwekwe ya striga inaadhiri shamba lako namna gani?**

Kwekwe ya striga inaingiza mizizi yake ndani ya mizizi ya mahindi au mtama.



Kwekwe inatumia chakula cha mahindi kutoka kwa udongo, kabla chakula hicho hakijafikia mmea wa mahindi.

### **Tunawezaje kuzuia striga?**

#### **Njia nyingi zilizopendekewa hazifanyi kazi.**

- Ng'oa kwekwe la striga na uchome nje ya shamba.
  - Hii ni kazi nyingi na ngumu lakini baadaye striga inarudi.
- Tumia dawa ya kuua kwekwe.
  - Njia hii ina gharimu pesa nyingi lakini baada ya muda kwekwe hurejea tena.
- Panda aina ya mahindi zinazovumilia striga.
  - Kwekwe haijapotea, njia hii ina kazi nyingi na mazao kila mara ni machache.
- Tia fatalaiza nyingi ili mahindi yatoe mazao mengi hata kama kuna striga.
  - Mbinu hii inagharimu pesa nyingi, kazi ni nyingi na kwekwe haijaenda.

### **HABARI NJEMA**

#### **Ni mbinu gani inayoweza kufanya kazi?**

Imegunduliwa kuwa ukipanda desmodium pamoja na mahindi unazuia striga kumea katika shamba la mahindi.



#### **Mbinu hii inafanya kazi namna gani?**

Mmea wa desmodium unafunika udongo wote kati ya mistari ya mahindi. Desmodium inatia aina ya kemikali isiyopendelewa na striga ndani ya udongo. Kwa hivyo, striga haitamea kule desmodium inakuzwa.

### **Kwa nini desmodium ni mmea mzuri?**

- Inazuia striga kumea.
- Inarudisha nitrogen ndani ya udongo.
- Ni malisho bora kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inafunika udongo wote, kwa hivyo, inazuia maji kupotea na inazuia mmomonyoko wa udongo.
- Baadhi ya wakulima watanunua mbegu yako ya desmodium kwa bei nzuri.

### **Mazao yataongezeka kwa kiwango gani?**

Ikiwa unavuna magunia kumi ya mahindi ukiwa na striga shambani bila striga utavuna hadi magunia kumi na tano ya mahindi na utakuwa na majani mabichi kwa mwaka mzima kwa ng'ombe wako wa maziwa.

### **Tunakuzaje desmodium pamoja na mahindi?**

Utapata mbegu ya desmodium kutoka:

- Kampuni za mbegu (kama Western Seed Co. Kenya Seed Co.)
- ICIPE, Mbita Point, Suba District
- Jirani wako aliyeanza kukuza desmodium.

Utahitaji karibu kilo moja kwa kila ekari.

Tayarisha udongo kwa uangalifu na ulainishe barabara.

Chimba mitaro katikati ya mistari ya mahindi. Tumia kijiti kilichochongwa.

